

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINISIA WAZEE NA WATOTO**

Anwani ya Simu: "AFYA", D'Salaam  
Simu Nambari: 2120261/7  
**Fax No. +255 22 2137591**  
Barua zote ziandikwe kwa Katibu Mkuu  
Unapojibu tafadhali taja:



6 Barabara ya Samora Machel  
S.L.P. 9083,  
**11478 DAR ES SALAAM.**

**Kumb. Na. HD 162/425/02/107**

**04 Januari , 2016**

Mkurugenzi,  
Hospitali ya Taifa Muhimbili,  
S.L.P. 65000,  
**DAR ES SALAAM.**

Wakurugenzi,  
Hospitali za Kanda za Rufaa (Mbeya, KCMC, Bugando)  
**Tanzania Bara.**

Wakurugenzi,  
Hospitali Maalum (ORCI, MOI, Kibong'oto, Mirembe)  
**Tanzania Bara.**

Waganga Wafawidhi,  
Hospitali zote za Rufaa za Mikoa,  
**Tanzania Bara.**

Waganga Wafawidhi,  
Hospitali zote za Wilaya,  
**Tanzania Bara.**

Waganga Wafawidhi,  
Zahanati, Vituo vya Afya nchini,  
**Tanzania Bara.**

**YAH: KUANDAA NA KUCHAPISHA KILA SIKU ORODHA YA DAWA  
ZILIZOKO KWENYE HOSPITALI, KITUO CHA AFYA NA  
ZAHANATI ILI WAGONJWA WAANDIKIWE**

Tafadhali husika na somo hapo juu.

Mhe. Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ameagiza kuanzia sasa Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati za umma kuanzisha utaratibu wa kuandaa na kuchapisha orodha ya dawa zinazopatikana katika hospitali zenu ili wagonjwa waandikiwe.

Orodha hiyo inatakiwa isambazwe kwa waganga na madaktari ili waweze kuwaandikia wagonjwa na kuondoa usumbufu kwani mara nyingi dawa mbadala huwa zinapatikana kwenye vituo vyenu vya huduma za afya.

Napenda niwakumbushe madaktari kwamba waandike majina halisi ya dawa (generic names) kama Sera ya Dawa inavyoagiza. Pia Kamati za Dawa na Tiba za Vituo vya kutolea huduma za afya zisimamie matumizi sahihi ya dawa na vifaa tiba.

Naagiza utekelezaji wa suala hili uanze mara moja mkiwashirikisha wafamasia walioko kwenye hospitali zetu na vituo vya afya ili azma ya serikali ya kutoa huduma bora kwa wananchi iweze kufikiwa.

Nawatakia kazi njema.



Prof. Muhammad Bakari Kambi  
**Kny: KATIBU MKUU**

Nakala:- Katibu Mkuu,  
Ofisi ya Waziri Mkuu,  
TAMISEMI  
Jengo la Mkapa,  
2 Barabara ya Nane  
S.L.P. 1923,  
**41185 DODOMA**